BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Pili – Tarehe 08 Mei, 2025

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2025/2026.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

138. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Lini nyumba ya makaazi ya muasisi wa Taifa la Zanzibar na Jemedari wa Mapinduzi ya Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume iliopo Kiongoni Mwera itafanyiwa ukarabati unaostahiki.

## Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

193. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

(a) Kwa mujibu wa sheria zilizopo ni aina gani ya mifuko ya plastiki hairuhusiwi kuingizwa, kusafirishwa, kuuzwa, kutengenezwa, kusambazwa na kuhifadhiwa.

(b) Kanuni zinazungumza vipi juu ya ruhusa au katazo la vifungashio vya plastiki.

(c) Kuna tofauti gani kati ya vifungashio vya plastiki na vibebeo vya plastiki.

## Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

257. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Lengo kuu la ukaguzi wa fedha za Serikali ni kuhakikisha kwamba fedha iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi inatumika kama ilivyokusudiwa.

Je, ni kwa kiasi gani Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) inawezeshwa katika kulifikia lengo hilo.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

33. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kituo cha Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) Sengenya Mtambwe ni miongozi mwa vituo vya muda mrefu vilivyopo katika Wilaya ya Wete. Pamoja na umuhimu wake katika operesheni za KMKM, ni kituo kilichosahauliwa katika miundombinu ya kisasa kama vile majengo na ofisi.

(a) Kwa kiasi gani uchakavu wa miundombinu ya Kituo cha KMKM Sengenya unakwamisha operesheni za KMKM.

(b) Je, ni lini Serikali itakikumbuka kituo hiki kwa kukipatia vifaa vya kisasa na majengo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

91. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Kwa kiasi gani Serikali inawapatia wajasiriamali mafunzo ya kuzalisha na kufungashia bidhaa zao.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

2. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Takwimu iko vipi juu ya mazingatio ya wanawake wenye mahitaji maalum katika ujenzi wa miradi ya kimkakati inayoendelea nchini.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

86. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Kwa kuwa mazao mengi hivi sasa yamekuwa na changamoto ya wadudu, je, kwa kiasi gani Wizara yako ina wataalamu wa kutosha wa maradhi ya wadudu wanaoshambulia mazao.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

299. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Serikali imetengeneza barabara kadhaa za ndani na nyenginezo kila kona lakini barabara nyingi zina kona zisizokuwa na ulazima.

    (a) Je, ni jambo gani lililopelekea kuwepo na kona nyingi zisizokuwa na ulazima.

    (b) Je, Washauri Elekezi na Wasimamizi wetu wa ndani walitoa maoni na miongozo gani kuhusiana na kona nyingi za barabara zetu.

**Wizara ya Afya:**

245. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika jimbo la Nungwi, shehia ya Kidoti kipo Kituo cha Afya katika kijiji cha Kidangoni, kilichomalizika kujengwa kwa miaka miwili sasa na Wizara ya Afya inalijua hili na imewahi kuombwa kutoa madaktari angalau wawili kwa ajili ya kutoa huduma kwa mama wajawazito na watoto wao.

(a) Je, ni lini kituo hiki kitapatiwa madaktari hao.

(b) Kwa kuhakikisha kuwa kituo hiki kipo na kimemaliza ujenzi, ni upi utayari wako wa kufuatana na mimi pamoja na wananchi kwenda kuthibitisha utekelezaji wa ahadi ya Wizara yako.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

103. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kipindi cha darasa huru ni miongoni mwa vipindi bora vinavyowapa hamasa vijana kuwa na uthubutu wa kujiajiri.

Je, Wizara yako inafanya jitihada gani ya kukiimarisha kipindi hiki ili kiweze kuwafikia wajasiriamali wengi waliopo Zanzibar.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

134. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Inasemekana mpaka sasa kuna mwitikio mdogo wa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika miradi ya umeme wa upepo, jua na mawimbi.

(a) Je, kuna ukweli gani wa suala hili.

(b) Ni sababu zipi zinazowakwamisha wawekezaji kuwekeza katika miradi hii.

III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2025/2026.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2025/2026.

Zanzibar,
08 Mei, 2025.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA